# SAUTI YA MANISPAA MOROGORO









# JARIDA LA MWEZI

## toleo namba 04

mwezi **novemba** 2020 - **februari** 2021

www.morogoromc.go.tz | YouTube Moromc online TV | Moromc

# MAGUFULI AWATAKA WAFANYABIASHARA SOKO KUU LA CHIFU KINGALU KUFANYA BIASHARA, WAKATI KERO ZAO ZIKISHUGHULIKIWA.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akizindua jiwe la msingi la soko kuu la Chifu Kingalu Morogoro.*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, amewataka wafanyabiashara wa Soko Kuu la Kingalu Manispaa ya Morogoro kuendelea kufanya biashara wakati kero na changamoto zao zikiendelea kushughulikiwa.

Hayo ameyazungumza Februari 11/2021, wakati akizindua Soko hilo ambalo limegharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 17.6.

Akizungumza na wananchi mara baada ya kuzindua Soko hilo,amesema Jumla ya Shilingi Bilioni 361 fedha za Serikali zimetumika katika ujenzi wa masoko ya kisasa 22 ambapo mpaka sasa ni masoko 9 ambayo yameshakamilika na mengine yako katika hatua za kukamilika.

Magufuli, amesema kuwa, katika masoko yote , Soko la Kingalu Manispaa ya Morogoro ni la kwanza likiwa limetumia Bilioni 17.6, likifuatiwa na Soko la Job Ndugai Dodoma Bilioni 14.6 na la tatu Soko la Kisutu Ilala Bilioni 13.4.

Hata hivyo baada ya kutembelea wafanyabiashara wa Soko hilo amekumbana na changamoto mbalimbali ikiwemo baadhi ya watu kupangishiwa na madalali kwa kiwango kikubwa cha fedha pamoja na tozo ya ushuru kwa mizigo inayoingia Sokoni.

“Nimepita kwa wafanyabiashara , kero zao zimenigusa sana, niombe Uongozi wa Mkoa wa Morogoro hizi changamoto zihakikishe zinapatiwa ufumbuzi haraka baada ya kuondoka, namuagiza Waziri Jaffo shughulikia haya mapema, na hakuna mfanyabiashara ambaye mzigo wake upo chini ya tani moja kutozwa ushuru” Amesema Magufuli.

INAENDELEA UK... 19

# WANANCHI WATAKIWA KUENDELEA KUSHIRIKI KATIKA UJENZI WA MADARASA.

Wananchi wametakiwa kuendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Serikali katika sekta ya elimu kwa kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika kutatua changamoto zinazoikabili sekta hiyo ikiwemo uhaba wa vyumba vya madarasa.

Akizungumza baada ya kukagua ujenzi wa vyumba nane vya madarasa vya Shule ya Sekondari Mkundi inayojengwa na nguvu za wananchi wa Kata hiyo wakishirikiana na Serikali,Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini Mhe.Abdulaziz Abood amesema ni wajibu wa kila mwananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo na kupongeza jitihada hizo za wananchi wa Kata ya Mkundi.

Baada ya kuridhishwa na jitihada hizo za wananchi wa Mkundi,Mhe. Abood amejitolea mifuko 125 ya saruji yenye thamani ya shilingi Milioni tatu na laki mbili na kuahidi kuendelea kushirikiana nao katika kufanikisha ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa.

Afisa Mtendaji wa Kata ya Mkundi na wananchi wa Kata hiyo wamemshukuru Mhe. Abood kwa kuwapatia msaada huo na wamesema kuwa shule hiyo kwa asilimia kubwa itasaidia kupunguza msongomano wa wanafunzi katika shule ya Sekondari Kingo ambayo inamilikiwa na Kata ya Kingo, na hii iliwafanya wanafunzi wa Kata ya Mkundi kulazimika kusoma katika shule hiyo kutokana na Kata yao kukosa Shule ya Sekondari.

Msaada huo alioutoa Mheshimiwa Abood ni mwendelezo wa utekelezaji wa ahadi zake na kuunga mkono jitihada za wananchi na Serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Jimbo la Morogoro mjini.



*Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini Mhe.Abdulaziz Abood akikabidhi mifuko ya saruji kwa Mtendaji wa Kata Laurent Masanja(aliyevaa tshirt nyeupe),kama mchango wake katika ujenzi wa Madarasa ya shule ya Sekondari Mkundi.*


# BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti ... Sheilla E. Lukuba**
*Mkurugenzi Manispaa ya Morogoro*

**Mhariri Mkuu ... Lilian K. Henerico**
*Afisa Habari Manispaa*

Washiriki wasaidizi

**Issa B. Issa:** *Afisa Habari Msaidizi*

**Yusuph A. Mwamba**
*Afisa Habari Msaidizi*



*mawasiliano:* *simu: 023 - 2935242*
*E-mail: info@morogoromc.go.tz*
*S.L.P 166*



*Mitandao ya Kijamii*

*Website:* *www.morogoromc.go.tz*
*youtube:* *Moromc online tv*
*instagram:* *Manispaa ya Morogoro*
*facebook:* *Manispaa ya Morogoro*

# WAHITIMU WA JESHI LA AKIBA (MGAMBO) WILAYA YA MOROGORO WATAKIWA KUWA WAZALENDO.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe.Bakari Msulwa, amewaasa vijana kuwa wazalendo wa nchi yao kwa kuacha kujiingiza katika viashiria vya uvunjifu wa amani ili kusaidia kuepukana na migogoro itakayopelekea uvunjifu wa amani.
Hayo ameyasema Novemba 25/2020 wakati wa kufunga rasmi mafunzo hayo yaliyofanyika katika uwanja wa Jamhuri Manispaa ya Morogoro.
DC Msulwa, amesema kuwa itakuwa ni fedheha kwa taifa ikibainika kuwa vijana hao waliopikwa kwa misingi ya uzalendo wakashiriki katika matukio ya ujangili na migomo isiyo na tija au kutumika kisiasa.
Katika hatua nyingine, amewapongeza wahitimu wote na kuwasihi kuyatumia mafunzo hayo kama chachu ya kujiletea maendeleo na kuhakikisha kuwa wanailinda jamii inayowazunguka.
Aidha, amewaahidi kuwa Serikali ipo nao bega kwa bega na ndiyo maana imetumia gharama kubwa kuwapatia mafunzo hayo.
Hata hivyo, ametumia fursa hiyo kuyaomba makampuni binafsi ya ulinzi kuwatumia vijana hao wenye mafunzo ya kijeshi kwa shughuli zao za ulinzi.
Pia, ametumia fursa hiyo kuwaasa vijana kuwa inapotokea fursa kama hiyo wajitokeze kwa wingi na wasikatishwe tamaa kwani Serikali inatumia gharama kubwa kufanikisha mafunzo hayo.

"Vijana wangu najua mmepitia vikwazo vingi na ninajua mlikatishwa tamaa maana wapo mabingwa wa kukatisha watu tamaa lakini mmevuka salama na leo mnahitimu, basi mafunzo haya yawe na tija katika maisha yenu binafsi na jamii inayowazunguka". Alisema DC Msulwa.

Mafunzo hayo ya miezi 4 yamejumuisha jumla ya Vijana 200 chini ya usimamizi wa Mshauri wa Jeshi la Akiba Wilaya ya Morogoro.



*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe.Bakari Msulwa akikabidhi zawadi kwa mmoja wa wahitimu wa mafunzo ya jeshi la akiba (mgambo)*



*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Loata Ole Sanare, akikagua eneo la mama lishe Soko kuu la Chifu Kingalu Manispaa ya Morogoro Januari 12,2021.*

# MEYA KIHANGA AWACHARUKIA WAALIMU WAKUU, AWATAKA WAJITATHIMINI.



Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, amewataka Walimu wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari, kujitathimini na kuona Kama wanafaa kukaa Manispaa Morogoro.

Kauli hiyo ameitoa Januari 19, 2021 wakati wa ziara ya kikazi ya ukaguzi wa ujenzi wa vyumba vya Madarasa vilivyojengwa na Manispaa Morogoro na nguvu za wananchi kufuatia agizo la Serikali la kutaka wanafunzi wote kuingia darasani ifikapo Februari 28.

Akizungumza mara baada ya ziara hiyo, Kihanga, amesema kumekuwa na matokeo mabovu ambayo hayaridhishi jambo linalopelekea Manispaa kushika nafasi za nyuma huku ikiwa hapaq ni mjini.

Mhe. Kihanga, amesema kuwa, sasa ni wakati wa Waalimu hao kuanza kujitathimini upya kutokana na matokeo hayo.

" Nimeanza ziara ya kikazi ya kukagua ujenzi wa Shule na vyumba vya Madarasa, lakini matokeo bado hayaridhishi hususani katika upande wa

INAENDELEA UK... 08

# MANISPAA YA MOROGORO YATOA MKOPO WA PIKIPIKI ZENYE THAMANI YA SHILINGI MILIONI 80 .

Manispaa ya Morogoro imetoa Mkopo wa Pikipiki wenye thamani ya Shilingi Milioni 80 kwa vikundi viwili vya bodaboda vya Bomsate pamoja na Twaweza Mindu.

Ugawaji huo wa Pikipiki umefanyika katika eneo la Stendi mpya ya Daladala Mafiga Desemba 01/2020.

Akizungumza na Waandishi wa habari, mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Albinus Mgonya ambaye ni DC wa Mvomero amevitaka vikundi mbalimbali kufanya kazi kwa uweledi jambo ambalo litasaidia vikundi hivyo kufanya marejesho ya fedha ili vikundi vingine venye uhitaji viweze kupata mkopo na kupiga hatua kimaendeleo.

Mhe. Mgonya amesema kuwa kama mikopo hiyo wataitumia kwa malengo yaliokusudiwa kwa muda mfupi wataweza kurejesha fedha kwa wakati na Manispaa itaweza kuwapa mikopo mingine.

“Leo tunatoa mkopo wa Bodaboda wenye thamani ya shilingi Milioni 80, tuvitumie vyombo hivi kwa malengo na turudishe fedha kwa wakati" Amesema Mgonya.

Ameeleza kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha wanawawezesha kiuchumi watanzania ili wawe na maisha mazuri jambo ambalo litaleta tija, kwani wataweza kujiajiri wenyewe kupitia mkopo huo.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaaa ya Morogoro, Pili Kitwana, amesema kuwa vikundi hivyo vinatakiwa kurejesha fedha kwa wakati ili wengine waweze kufaidika na mikopo

INAENDELEA UK... 12

# POLEPOLE ATAKA ZOEZI LA UHAKIKI WA WAFANYA-BISHARA SOKO KUU MANISPAA YA MOROGORO KUFANYIKA UPYA.

Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM Taifa (Mb), Mhe. Humphrey Polepole, ameuagiza Uongozi wa Manispaa ya Morogoro kuanza upya zoezi la uhakiki wa Wafanyabiashara waliosajiliwa katika Soko hilo ili kubaini wenye sifa na wasio na sifa.

Kauli hiyo ameitoa Januari 10, 2021 , wakati wa ziara ya kusikiliza na kutatua kero katika Soko hilo mara baada ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya awamu ya tano katika Manispaa ya Morogoro na mradi wa SGR ambao upo katika hatua za mwisho kukamilika.

Akizungumza na Waandishi wa Habari , Mhe. Polepole, amemtaka Mkuu wa Wilaya ya Morogoro kwa kushirikiana na Mstahiki Meya , Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro na Ofisi ya CCM Wilaya kwa kutumia Kamati ya Soko waanze kufanya uhakiki upya wa wafanyabiashara waliosajiliwa katika Soko hilo ili kubaini wale wenye sifa na wasio na sifa.

"Nataka zoezi hili la uhakiki wa kizimba kwa kizimba,fremu mojamoja kwa kila mfanyabiashara ili kuhakikisha kweli ni mtu mmoja na kizimba kimoja au fremu, nafahamu watu waliomba vizimba, na fremu za biashara , na Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro alielekeza na kuwakumbusha kwamba ikifika tarehe 5 Januari , 2021, kila mwenye kizimba awe amefika eneo lake, hivyo kwa tarehe aliyotangaza Mkurugenzi na leo ni tarehe 10, sasa tunawatakia kilalakheri wale wenye vizimba ambao hawajafika katika eneo lake. Soko hili ni kubwa sana lakini ni kama ndoo ya maji ina jaa tungetamani kila mtu awe hapa lakini haiwezekani" Amesema Mhe. Polepole.

Mhe. Polepole , ametoa maelekezo kwa Uongozi wa Manispaa ya Morogoro kwamba kwa wale walioshika vizimba viwili uwekwe utaratibu mzuri ili hao waliokosa wapatiwe maeneo ambayo wataweza nao kufanya biashara zao.

Mwisho, amewatahadharisha wale wenye tabia ya kupangisha vizimba kwa mfanyabiashara mwengine kuacha tabia hiyo kabla ya sheria kuchukua hatua kali.

Kwa upande wa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Bakari Msulwa, amesema hawatawavumilia wale watakaokutwa wana vizimba zaidi ya viwili kwani licha ya kuwa na kero za msingi na manung'uniko lakini kuna haja ya



*Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM Taifa (Mb) Mhe. Humphrey Polepole(katikati),Mhe.Pascal Kihanga(kulia),mhandisi wa ujenzi Manispaa Juma Gwisu wakiwa katika ziara ya ukaguzi wa soko kuu la kisasa Manispaa ya Morogoro.*

kuangalia kwa jicho pana changamoto hizo ili pande zote ziweze kuwa kitu kimoja kwa maendeleo ya Manispaa ya Morogoro.

" Ni kweli kuna changamoto nyingi katika Soko letu, kuna hoja za msingi za wafanyabiashara wa ndani na nje, tumejitahidi kupunguza kero lakini hatukuzimaliza, kama alivyosema mwenezi sasa tunakwenda katika hatua kubwa, hili ni kweli lina changamoto nyingi, lakini tumejitahidi kupunguza kero,lakini nimetengeneza timu kubwa ya kushughulikia kero hizi tunaimani tutazimaliza taratibu taratibu, wiki inayoanza kuanzia tarehe 11 Januari kamati itakuwa hapa kumsikiliza kila mdau lakini nawaomba tuwe wakweli na kuwa waaminifu katika jambo hili " Amesema DC Msulwa.

DC Msulwa, amesema lazima kazi ifanyike kwakuwa fedha zilizojengea Soko hilo ni za walipa kodi.

# WAITARA ARIDHISHWA NA USAFI MANISPAA YA MOROGORO, ATAKA KASI IONGEZWE KATIKA UPATIKANAJI WA DAMPO LA KISASA.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Mwita Waitara, ameipongeza Manispaa ya Morogoro kwa mipango mizuri na usimamizi mzuri wa usafi huku akitaka nguvu iongezwe katika ufuatiliaji wa upatikanaji wa dampo la Kisasa.
Kauli hiyo ameitoa wakati wa ziara ya ukaguzi wa dampo la taka Manispaa ya Morogoro lililopo Kata ya Mafisa.



*Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mhe. Mwita Waitara (katikati) akizungumza na watumishi wa Manispaa mara baada ya kuwasili katika eneo la kuhifadhia taka(dampo) katika ziara yake ya kikazi*

"Nimefurahishwa sana na hatua za kuanza kutekeleza ujenzi wa dampo la Kisasa, mmeniambia tayari andiko lipo na mshaliwasilisha kazi yangu mimi ni kusukuma ili hizo fedha zitoke, lakini niwaombe dampo la kisasa lizingatie miundombinu yote, lisiwe kama hili la kienyeji,mhakikishe mnajiandaa vyema na ujenzi wa dampo Jipya , hili tulilo nalo tuliwekee mazingira rafiki taka zisibaki nje, hapa kuna taka ambazo zinazalisha sumu, haya maji yakitiririka yanawafikia wananchi na ni hatari kwa afya"Alisema Waitara.
Aidha, amesema sio jambo baya Manispaa ikafanya ziara kwa ajili ya mafunzo na kuona wenzenu walivyojipanga katika ujenzi wa madampo pia usafishaji wa Mji .
Mhe. Mwita, amesema

INAENDELEA UK... 21

# DC MSULWA AWATAKA WANANCHI KUITUNZA MIUNDOMBINU ILIYOPO.




*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe.Bakari Msulwa (kulia), akizindua kituo cha Daladala Kaloleni Novemba 6/2020 , (kushoto) Michael Waluse kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro.*

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Bakari Msulwa, amewataka Wananchi kutunza miundombinu iliyopo katika maeneo yao kwa sababu fedha za matengenezo ya miradi hiyo zinatokana na kodi zao.

Kauli hiyo ameitoa Novemba 06/2020, wakati wa uzinduzi wa Stendi ya Daladala ya Kaloleni iliyopo Kata ya Mji Mpya Manispaa ya Morogoro. Msulwa, amesema kuwa licha ya kuwa ni haki yao, njia moja wapo ya kuthamini fedha zao ni kulinda miundombinu iliyopo na inayoendelea kujengwa.

"Tatizo kubwa tulilo nalo ni kushindwa kutambua haki na wajibu wetu kama walaji,ndiyo sababu inayotufanya kugharamia vitu ambavyo kama tungevitunza vizuri tusingetarajia kupata gharama hizo, kwahiyo ni wajibu wetu kuthamini fedha zetu maana zinatokana na kodi zetu wenyewe " Aliongeza DC Msulwa.

"Manispaa ya Morogoro ni Mji Kongwe sana , kwa hili lililofanyika leo naupongeza sana Uongozi wa Manispaa ya Morogoro kwa kuonesha na kuufanya Mji huu kuwa sura ya Manispaa, lakini niseme unapokuwa na uongozi mzuri ngazi ya Kitaifa, Jimbo na Kata unatengeneza uelekeo mzuri wa kutengeneza maendeleo kwa wananchi au taasisi husika, kwahiyo uchaguzi umekwisha, matokeo tumeyasikia na Viongozi wetu wameshaanza kufanya kazi" Amesema Msulwa.

Aidha, amesema lengo la Manispaa hii ni kuwa Jiji hivyo ni lazima miundombinu iweze kuboreshwa licha ya kuwa zipo changamoto zitakazo jitokeza.

"Hatuwezi kukaa katika Manispaa kwa miaka 32 na tukaendelea kukaa kwa muda mrefu kabla ya hatujafika kiwango cha kuwa Jiji, lakini ukishakuwa Jiji lazima utarajie changamoto mbalimbali, changamoto hizo pia zinaweza kugeuka kuwa fursa , kwahiyo hatua ambazo Manispaa imezichukua zinatufanya kuelekea kuwa Jiji, nafahamu ukiachia stendi hii ya Kaloleni, kuna Stendi kuu ya daladala Mafiga, Soko kuu la kisasa, na miradi mingine ambayo inaendelea nawapongeza sana Manispaa, wahandisi wa miradi kwa kazi kubwa na nzuri mnazo fanya",Ameongeza DC Msulwa.

Pamoja na hayo amesema ni

INAENDELEA UK... 11

# MEYA KIHANGA AWACHARUKIA WAALIMU WAKUU, AWATAKA WAJITATHIMINI.

INATOKA UK... 04

Sekondari, tunashindwa hadi na wenzetu wa vijijini, sisi tuna kila kitu ila ni wapi tuna kwama? Hizi nafasi sio zetu, niwaombe Waalimu mjitathimini, Serikali inawekeza katika ujenzi na sisi tunataka matokeo mazuri, baada ya ujenzi wa madarasa tunahamia kwenu, kama umeshindwa kukaa Manispaa ondoka kabisa, tunataka matokeo mazuri tufanane na hadhi yetu ya Manispaa" Alisema Mhe.Kihanga.

Aidha aliwataka Waalimu wakuu wanapokaa katika vikao vyao wamualike ili wazungumze kwa pamoja na kuona changamoto ambazo zipo na kuzitatua. Suala la Waalimu amesema kuwa mpango uliopo kwa sasa ni kuongeza Waalimu wa Sayansi ambao ndio changamoto kwa Sasa. Kuhusu Ujenzi wa Shule ya Msingi Konga, amempongeza Sana Mkurugenzi Manispaa Morogoro Sheilla Lukuba, kwa jitihada za kupambania Sekta ya elimu, kwani Sasa amekuwa akitoa fedha nyingi katika kata kwa ajili ya maendeleo mbalimbali ikiwemo sekta ya elimu.

" Mkurugenzi wetu anajitahidi Sana , tumtumie vizuri, anahangaika Sana, sisi hatuhitaji kubweteka, tufanye kazi, haya matokeo yanatuumiza Sana, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wote tunaumia, huu ni muda wa kujipanga sasa tutoke hapa tulipo twende mbele"Aliongeza Mhe. Kihanga.

Mwisho , amesema kuwa ziara hizo zitakuwa endelevu, lakini kwanza ameanza katika Shule za Sekondari baada ya hapo atahamia Shule za Msingi. Miongoni mwa Shule alizoanza nazo ziara ni pamoja na Shule ya Msingi Konga Kata ya Mzinga, Shule ya Sekondari Kihonda Kata ya Mazimbu, Shule ya Sekondari Sumaye Kata ya Bigwa na Shule ya Sekondari Lupanga Kata ya Kilakala.

Naye Diwani wa Kata ya Kilakala, Mhe. Marco Kanga, amemshukuru, Mstahiki Meya kwa ziara hiyo huku akimuahidi kumpa ushirikiano na kuhakikisha anafuatilia kwa ukaribu maswala ya elimu katika Kata hiyo.

# DC MSULWA, AONGOZA MAMIA YA WANANCHI KATIKA KAMPENI YA KUPANDA MICHE YA MITI 15,000 PEMBEZONI MWA BWAWA LA MINDU MANISPAA YA MOROGORO.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro. Mhe. Bakari Msulwa, ameongoza mamia ya wananchi wa Manispaa ya Morogoro zikiwemo Taasisi za Serikali na za watu binafsi kushiriki katika Kampeni ya Kupanda Miche ya Miti 15,000 pembezoni mwa Bwawa la Mindu Manispaa ya Morogoro .

Zoezi hilo la Kampeni ya upandaji wa Miti pembezoni mwa Bwawa la Mindu Manispaa ya Morogoro limefanyika Desemba 09/2020 ikiwa ni Sherehe ya kutimiza miaka 59 ya Uhuru wa Tanzania.



*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro. Mhe. Bakari Msulwa akipanda mti katika Kampeni ya Kupanda Miche ya Miti 15,000 pembezoni mwa Bwawa la Mindu Manispaa ya Morogoro tarehe 9/12/2020.*

Akizungumza na viongozi mbalimbali pamoja na wananchi walioshiriki katika zoezi hilo, DC Msulwa, amesema kuna umuhimu mkubwa na faida katika utunzaji wa mazingira hususani kupanda miti pembezoni mwa Mito na mabwawa ambapo faida zake

INAENDELEA UK... 13

# MADIWANI MANISPAA YA MOROGORO WATAKIWA KUBUNI VYANZO VIPYA VYA MAPATO.



*Waheshimiwa Madiwani wa Manispaa ya Morogoro wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa uzinduzi wa Baraza Jipya la Madiwani*

Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Emmanuel Kalobelo, amewataka Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuboresha vyanzo vilivyopo ili kuiwezesha Halmashauri kuongeza uwezo wa kujitegemea kwa mapato ya ndani.

Kalobelo, ameyasema hayo katika mkutano wa Uzinduzi wa Baraza la Madiwani uliofanyika Desemba 14,2020 katika Ukumbi wa Mikutano uliopo Stendi ya Mabasi Msamvu.
Amesema kuwa Halmashauri ikiboresha mapato itasaidia kuweza kutoa huduma za kijamii kwa wananchi ikiwemo afya, elimu, Maji n.k na pia kiwango cha mikopo kwa vikundi vya vijana,wanawake na watu wenye ulemavu itaongezeka.
Hata hivyo, amewataka Waheshimiwa Madiwani kutenga maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya viwanda vidogo, vya kati na vikubwa kufanya hivyo kutaongeza Mapato ya Halmashauri na Serikali kuu.
Hata hivyo, amesema kuwa ukusanyaji wa mapato ya ndani lazima uendane na nidhamu ya matumizi ya fedha kwa hiyo ni jukumu la Baraza la Madiwani kusimamia na kuhakikisha kuwa mapato yote yanayokusanywa katika vyanzo vya ndani yanatumika ipasavyo.

"Nitoe rai kwa Manispaa , hakikisheni fedha zinazokusanywa kutoka katika vyanzo vya mapato zisitumike zikiwa mbichi, bali zinatakiwa kupelekwa benki na kutumika kwa kufuata utaratibu mzuri na ulio sahihi kisheria" . Amesema Eng. Kalobelo.

" Nipongeze Baraza la Madiwani kwa kweli mmefanya vizuri sana katika kipindi cha miaka 5 iliyopita , sasa tunataka uwepo wa Baraza Jipya uwe chachu kubwa ya maendeleo, tutawapima baada ya miaka 5, yapo maendeleo mmeyakuta, tunataka muyaendeleze na kuanzisha mapya, lakini tusisahau wafanyabiashara kuwajengea mazingira mazuri, lazima tuhakikishe kwamba tunajenga kituo cha One Stop Centre kwa ajili ya wafanyabiashara wote" Ameongeza Eng. Kalobelo.
Aidha Eng.Kalobelo, amewataka Viongozi kuendelea kuhamasisha Wananchi kujiunga na Bima ya afya ya CHF iliyoboreshwa huku Serikali ikiwa na kazi ya kuhakikisha kwamba dawa na vifaa tiba vinapatikana kwa uhakika ili kuendelea kuboresha afya na Ustawi wa Wananchi.

Mwisho, aliwataka Wah.Madiwani kuhakikisha wanakamilisha Ujenzi wa vyumba 26 vya Madarasa mapya na Madawati yake kabla ya mwezi Februari 2021 ili wanafunzi wapate kukaa na kusoma vizuri.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Bakari Msulwa, amewapongeza Manispaa ya Morogoro kwa ufaulu wa Wanafunzi Kidato cha kwanza ambapo kwa Manispaa Jumla ya Wanafunzi 7,577

INAENDELEA UK... 14

# MANISPAA MOROGORO YAIBUKA KINARA WA LISHE MKOA WA MOROGORO.



*Afisa Lishe Manispaa ya Morogoro Elina Kweka akisalimiana na Katibu Tawala Mkoa Mhandisi Emmanuel Kalobelo mara baada ya kukabidhiwa cheti cha shukrani cha ushindi wa kwanza kimkoa katika maswala ya Lishe*

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro Februari 03/2020 , imeibuka kuwa kinara wa lishe katika Mkoa wa Morogoro ikifuatiwa na Halmashauri ya Mvomero na Kilosa.

Akizungumza mara baada ya kupokea ushindi huo wa cheti cha shukrani kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Afisa Lishe Manispaa ya Morogoro Elina Kweka,amesema ushindi huo umeifanya Manispaa kuanza kuongeza kasi zaidi ya kupambana na changamoto za lishe duni kwa watoto.

Kweka, amesema kuwa,watahakikisha kwamba wanaongeza uelewa na matokeo chanya kwa jamii ili kukabiliana na changamoto za afya na lishe zinazowakabili watoto. “Tumepokea cheti cha shukrani cha kuwa kinara wa lishe kimkoa, lakini ushindi huu umechangiwa na watu wengi , kwanza kabisa nimpongeze Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro kwa kutenga fedha ambazo zimekuwa zikisaidia katika lishe, Baraza la Madiwani la Manispaa , Mganga Mkuu wa Manispaa , Afisa Maendeleo ya Jamii Manispaa, wadau wa lishe, pamoja na watoa huduma ngazi ya jamii na ngazi ya vituo vya kutolea huduma, kwakweli wamefanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha Manispaa ya Morogoro inatokomeza watoto wenye udumavu, ombi langu endeleeni kupambana ikiwa ni pamoja na kutoa elimu mara kwa mara ili huduma hii iweze kutekelezeka vizuri katika Jamii”Amesema Kweka.

# DC MSULWA AWATAKA WANANCHI KUITUNZA MIUNDOMBINU ILIYOPO.

INATOKA UK... 07

vizuri pia Mkurugenzi wa Morogoro Vijijini kufika hapa na timu yake ya uongozi ili nao waweze kujifunza na wao wakajenge stendi kama hii kwa ajili ya kurahisisha huduma za usafiri kwa wananchi wao. Mwisho , DC Msulwa, aliahidi kiasi cha Shilingi Milioni Moja kwa ajili ya ukarabati wa Kituo kidogo cha Polisi cha Mji Mpya.

Naye Kaimu mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Michael Waluse, ameshukuru kwa pongezi zilizotolewa katika ofisi yake, ameahidi kushirikiana na uongozi wa daladala wa stendi hiyo kwa yale yote yatakayojitokeza katika stendi hiyo.

Waluse, amesema kuhusu ukarabati wa kituo kidogo cha Polisi kilichopo jirani na Stendi hiyo, suala hilo litajadiliwa katika vikao na kuona ni jinsi gani Manispaa itakavyoweza kushiriki katika ukarabati ili kituo hicho kiwe na hadhi ya stendi hiyo kwani Jeshi la Polisi ndio watu wa kwanza katika kulinda amani katika eneo hilo.

Kwa upande wa Msimamizi wa fedha za mkopo wa Benki ya Dunia chini ya fedha za uboreshaji Miji ( Urban Local Government Strengthening Program (ULGSP) na Mhandisi wa TARURA Manispaa ya Morogoro, James Mnene, amesema mradi huo umegharimu kiasi cha Shilingi milioni 644 ambapo ujenzi wake ulianza Aprili 28/2020. "Mkandarasi Nandhra amekamilisha Ujenzi huo kwa asilimia mia moja kama ilivyoonekana wakati wa ukaguzi kabla ya kuzinduliwa, na mpaka sasa Mkandarasi ameshalipwa shilingi milioni 566 sawa na asilimia 74.9 na kiasi kilichobakia atalipwa baada ya kuwasilisha madai yake ya mwishoni na matumaini ya Manispaa ya Morogoro katika Stendi hii ya Daladala ni kutoa huduma bora ya usafiri kwa magari ya Daladala yapatao 50 na kuongeza Manispaa mapato" Amesema Mnene.

.Hata hivyo, Diwani mteule wa Kata ya Mji Mpya, Emmy Kiula, amemshukuru Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Bakari Msulwa , kwa kukubali ombi lake la kukarabati Kituo kidogo cha Polisi cha Kata ya Mji Mpya kufuatia Mkuu wa Wilaya kuahidi kiasi cha Shilingi Milioni moja.

Mwenyekiti wa umoja wa madereva wa daladala Mkoa wa Morogoro, Hemed Ntengwa, amesema Stendi hiyo ilikuwa changamoto sana lakini kwa sasa watafanya kazi vizuri na kuitunza miundombinu ya stendi hiyo.



*Muonekano wa stendi mpya ya Kaloleni iliyozinduliwa Novemba 6 2020*

INAENDELEA UK... 18

# MANISPAA YA MOROGORO YATOA MKOPO WA PIKIPIKI ZENYE THAMANI YA SHILINGI MILIONI 80 .

INATOKA UK... 04

inayotolewa ndani ya Manispaa Morogoro.
Kitwana,amesema kuwa pikipiki walizotoa wamezikatia bima kubwa ili kuhakikisha vikundi hivyo wanafanya shughuli zao katika mazingira rafiki na kupata faida.
Amesema kuwa mpaka sasa vikundi vyote wamewapatia elimu ya kurejesha mikopo kwa wakati, huku akifafanua kuwa kama watazitunza vizuri wataweza kununua za kwao wenyewe baada ya miaka 5.
Naye Afisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Morogoro, Enedy Mwanakatwe, amesema kuwa zoezi la kutoa mikopo ya bajaji na Pikipiki ni sehemu ya kutimiza ndoto ya Mhe.Rais Dkt. John Pombe Magufuli katika kuhakikisha kila mtanzania anakua na maisha mazuri.
Hata hivyo vikundi vilivyopata mikopo hiyo wameonekana kuwa na furaha huku wakiaidi kwenda kufanya kazi kwa ufanisi kwa ajili ya kupiga hatua za kimaendeleo.
Miongoni mwa vikundi vilivyopata mkopo ni pamoja na Mindu twaweza pikipiki 7 pamoja na Bomsate pikipiki 30 ambapo jumla ya pikipiki ni 37.



*Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Albinus Mgonya ambaye ni DC wa Mvomero(aliyevaa suti)akiwasha pikipiki mara baada ya kuwakabidhi pikipiki 37 kwa vikundi vya Boomsate na Twaweza Mindu tarehe 1/12/2020 katika eneo la stendi ya daladala Mafiga.*

# DC MSULWA, AONGOZA MAMIA YA WANANCHI KATIKA KAMPENI YA KUPANDA MICHE YA MITI 15,000 PEMBEZONI MWA BWAWA LA MINDU MANISPAA YA MOROGORO.

INATOKA UK... 08

ni pamoja na kupata hewa safi, mvua za kutosha , kivuli, kutumika kama mipaka na kulinda vyanzo vya maji .
Aidha, amesema katika kumbukizi ya miaka 59 ya Uhuru , Wilaya yake zikiwemo Halmashauri zote mbili zimeandaa kampeni hiyo ya kupanda miti ili kulinda vyanzo vyake vya maji na kuendelea kutoa huduma bora ya Maji kwa wananchi.

"Nimefurahishwa sana na Kampeni hii, kwani vyanzo vyetu vya maji hali si nzuri watu wanafanya shughuli za kiuchumi katika vyanzo hivyo, wengine wanaziba vyanzo, sasa nimeambiwa Bwawa letu lina miaka 40, unafikiri kama tungeanza uharibifu nyuma tungekuwaje? Niwaombe tuache shughuli katika vyanzo vya maji, Bwawa lina jaa matope , tumeanza naomba wale wenye mashamba tuliyopanda miti watusaidie kusimamia miti hiyo ikue, ugomvi wetu utaanza hapa haiwezekani mazao yako yanakuwa na miti yetu inakufa wakati ipo katika shamba lako, nitoe wito tusiishie hapa kila mtu anawajibu wa kulinda vyanzo vya maji ili tuendelee kupata huduma hii" Amesema DC Msulwa.

"Pamoja na yote, nimefurahishwa sana na ujio wa wageni wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutoka Jimbo la Mwanakwerekwe Zanzibar, hii imeonyesha ni jinsi gani Muungano wetu ulivyo na thamani kubwa ndani ya Taifa hili, tunaomba tuuenzi Muungano wetu kwani unafaida kubwa sana kwa Taifa letu na Maendeleo yetu " Ameongeza DC Msulwa.

Katika hatua nyingine, DC Msulwa, ametoa wito kwa Wazazi kuhakikisha ifikapo mwakani kila mzazi anapomwandikisha mtoto shule na wale wanaaonza kidato cha kwanza kufika shuleni hapo akiwa na mche mmoja wa mti ili kuweka mazingira yenye ukijani.

Kwa upande wa Brigedia Jenerali , Mkuu wa Kikosi cha Jeshi la Mazao kikosi cha Mzinga, Seif Hamisi, amewaasa washiriki na wananchi kujali mazingira ya sehemu wanazofanyia kazi na kuahidi kuwa miti hiyo iliyopandwa itatunzwa na kulindwa ipasavyo kwa kushirikiana na Uongozi na Wananchi wa eneo la Bwawa la Mindu ambapo ndipo Kambi ya Mzinga ilipo.

"Tunataka Kampeni hii ya upandaji wa miti iwe endelevu ili kuhakikisha Mindu inapokea maji mengi kutoka katika vyanzo vya maji pamoja na kurudisha Mindu katika ukijani wake unaotakiwa kwani Mindu ya Kijani inawezekana" Amesema Brigedia Jenerali Seif.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Michael Waluse, amesema Manispaa ya Morogoro haipo nyuma ambapo wana wadau ambao wameingia nao mkataba wa kila mwaka kuwapatia miche kwa ajili ya kupanda.

Waluse, amesema Ofisi ya Manispaa ipo wazi inashirikiana na wadau wote wa Mazingira ikiwa na lengo la kuweka Mji safi pamoja na kutunza vyanzo vya maji visiweze kuharibiwa kutokana na shughuli za kiuchumi zinazofanywa na wananchi.

" Kwa upande wetu Manispaa ya Morogoro, tunakusudia kupanda miti mingi kwani licha ya kuwa ni agizo la Makamu wa Rais wa Tanzania, Mhe. Mama Samia Suluhu pia ni faida kwa vizazi vijavyo" Alisema Waluse.

Naye, Mkurugenzi wa MORUWASA Manispaa ya Morogoro, Mhandisi Tamim Katakweba, amemshukuru Mkuu wa Wilaya Mhe. Bakari Msulwa pamoja na Bregedia Jenerali ,Seif Hamisi ambaye ni Mkuu wa Kikosi cha Jeshi Mazao Mzinga , kwa kukubali kuhudhuria uzinduzi huo wa Kampeni ya kupanda miti

ambapo awamu ya kwanza imepandwa miche ya miti 15000 kati ya miche ya miti ya miche 500000 iliyopangwa kupandwa katika eneo hilo la pembezoni mwa Bwawa la Mindu.

"Leo tumeshuhudia Mkuu wetu wa Wilaya akiongoza Kampeni ya upandaji wa Miti, viongozi na wananchi wamepanda miti ikiwa ni uzinduzi wa Kampeni ya upandaji wa miti katika Vyanzo vya Maji Wilaya ya Morogoro inayosimamia na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa ya Morogoro , Ofisi ya Bonde la Mto Ruvu, Ofisi ya Idara ya Misitu pamoja na sisi watu wa MORUWASA, niendelee kuchukua nafasi hii kuwaomba wale wakazi wanaofanya shughuli mbalimbali katika ukanda huu wa pembezoni mwa Bwawa watusaidie kuhakikisha kwamba wanakuwa nje ya Mita 60 lakini wajitahidi kutunza miti hii ambayo ipo katika mashamba yao" Amesema Eng. Tamim.

Katika hatua nyengine, Eng. Tamim, amesema MORUWASA imetenga kiasi cha fedha chenye thamani ya shilingi Bilioni 185 kwa ajili ya maboresho ya huduma za maji Manispaa ya Morogoro ikiwamo kupanua Bwawa la Mindu pamoja na kununua mtambo mpya.

# MADIWANI MANISPAA YA MOROGORO WATAKIWA KUBUNI VYANZO VIPYA VYA MAPATO.

INATOKA UK... 14

wamefaulu kujiunga na Kidato cha kwanza.

Amesema kazi iliyopo mbeleni ni kuhakikisha wanatekeleza agizo la Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, la kuhakikisha hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Februari , 2021 Wanafunzi wote waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza wanaanza masomo wakiwa Madarasani na wakiwa wamekalia Madawati yao.

Msulwa, amesema darasa moja linajumla ya thamani ya Shilingi Milioni 20, hivyo Manispaa itahitaji kutumia Shilingi Milioni 520 kujenga madarasa mapya 26 bila kujumuisha ukamilishaji wa Maboma na samani zake.

" Ndugu zangu , leo mmekula viapo na mmezindua Baraza jipya , katika agizo hili tuna siku 74, za kujenga Majengo 26 mapya na kumalizia maboma 13 ambapo madarasa hayo yanatakiwa kukamilika na watoto wawe madarasani, hili ni agizo la Serikali, tusianze vibaya kwa kushindwa kutekeleza agizo hili rasmi la Serikali Kuu, kila siku lazima tulifanyie kazi , Mkurugenzi na Madiwani tusikae kimya angalia kama kwenye Kata yako kuna Sekondari, licha ya fedha za Manispaa, lakini tumeandaa utaratibu mzuri wa kukusanya michango kutoka kwa wadau wetu mbalimbali wa maendeleo ili kufanikisha zoezi hili , peke yetu hatuwezi , ni lazima tushirikiane na wadau wetu " Amesema DC Msulwa.

"Nawaomba sana Waheshimiwa Madiwani tumpe ushirikiano Mkurugenzi wa Manispaa yetu, katika kipindi kifupi nilichofanya naye kazi nimegundua kuwa mkishikamana naye kasi yetu ya Maendeleo itaongezeka sana, mimi naamini mkitumia uwezo wake na kujiepusha na migongano isiyo na tija, Morogoro itaingia katika hadhi ya Jiji ikiwa mpya kabisa, Hongereni sana Manispaa, chapeni kazi, " Ameongeza DC Msulwa.

Kwa upande wa Katibu Tawala Wilaya ya Morogoro, Ruth John, amewataka madiwani hao kuwa na umoja na mshikamano katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowasilishwa kwao kutoka kwa wananchi ili kuweza kuzitatua na kuzijadili kwa pamoja.

Naye Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, amesema atafanya kazi bila ubaguzi wowote hivyo ameomba madiwani wote kumuunga mkono katika harakati za kuleta Maendeleo Jimbo la Morogoro Mjini. "Tufanye kazi kwa pamoja, mimi siko upande wa mtu yeyote, Bali nahusiana na watu wote kikubwa ni kuleta Maendeleo ndani ya Hal-

mashauri yetu ya Manispaa ya Morogoro na tuvunje makundi kinachotakiwa ni kwenda kuitekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi CCM kwa vitendo kama tulivyo ahidi kwa Wananchi " Amesema Mhe. Abood.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, amehimiza umoja na mshikamano baina ya madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ili kuweza kuwatumikia vyema wananchi wa Manispaa ya Morogoro.

Mhe. Kihanga, amesema baada ya uchaguzi huo kumalizika viongozi wanajukumu na wajibu wa kuwatumikia wananchi wao bila kuchoka ili kuleta maendeleo yao na hatimaye kuweza kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi.

# HABARI PICHA KUONESHA MATUKIO MBALIMBALI.



*Muonekano wa jengo la Soko kuu Chifu Kingalu Morogoro*




*Wanafunzi waanzilishi wa Shule ya awali ya mchepuo wa Kingereza Mji Mkuu Pre & Primary Manispaa ya Morogoro wakiwa katika picha ya pamoja.*



*Muonekano wa jengo la Shule mpya ya Serikali yenye mchepuo wa kingereza Mji mkuu pre & primary school inayomilikiwa na Manispaa ya Morogoro.*

# WAZAZI WAASWA KUTOA MALEZI BORA KWA WATOTO ILI KUTIMIZA NDOTO ZAO.

Wazazi wameaswa kuchukua hatua madhubuti ya kuhakikisha watoto wanapatiwa malezi bora na mahitaji yao muhimu ili waweze kutimiza malengo yao na kufikia ndoto zao.
Kauli hiyo imetolewa na Afisa Ustawi wa Jamii Manispaa ,Sidna Mathias, katika kilele cha maadhimisho ya Siku 16 za kupinga Ukatili wa Kijinsia ambapo kwa Manispaa ya Morogoro maadhimisho hayo yalifanyika katika viwanja vya Ofisi ya Kata ya Kihonda Desemba 10/2020.
Akizungumza na washiriki katika maadhimisho hayo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro , Sidna, amesema kuwa suala la ulinzi na usalama wa watoto sio suala la Serikali pekee bali ni suala la kila mzazi kuhakikisha ulinzi na usalama wa watoto unazingatiwa .




*Afisa Ustawi wa Jamii Sidna Mathias akizungumza wakati wa kilele cha maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili, disemba 10, 2020.*

"Leo tuna hitimisha kilele cha Siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia , niwaase wataalamu waendelee kutoa elimu hii ya ukatili wa kijinsia ili tuweze kupunguza au kutokomeza kabisa matukio ya ukatili katika jamii yetu, lakini tujitahidi kufichua matendo yote ya ukatili na taarifa zetu tuzitoe kwa siri ili wale wahusika waweze kuchukuliwa hatua kali za kisheria " Alisema Sidna.
Sidna, alisema lengo la maadhimisho hayo ni kujenga uelewa wa pamoja kwa Jamii juu ya ukatili na madhara yake hususani kwa wanawake na watoto pamoja na jinsi ya kuzuia ukatili wa kijinsia usiendelee kuwa janga miongoni mwa Jamii.
Aidha alieleza kuwa Manispaa ya Morogoro kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo, CVM, Boresha Afya, Morogoro Parallegal na Polisi Dawati la Jinsia katika kuelekea kilele hicho imeku-

INAENDELEA UK... 23

# HABARI PICHA KUONESHA MATUKIO MBALIMBALI.



Mkurugenzi Manispaa ya Morogoro Sheilla Lukuba, akigonga chiazi na Mkuu wa Wilaya ya Morogoro , Mhe.Bakari Msulwa, wakati wa uzinduzi wa Mnada wa nyama choma Kata ya Tungi. Uzinduzi ulifanyika Oktoba 14/2020.



Muonekano wa shule mpya ya Msingi Konga iliyojengwa Kata ya Mzinga.



Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood (katikati) akikagua eneo la wafanyabiashara wa mboga na vitoweo Soko Kuu la Kisasa Manispaa ya Morogoro, (kushoto) Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro , Sheilla Lukuba.

# HABARI PICHA KUONESHA MATUKIO MBALIMBALI.




*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Bakari Msulwa (aliyevaa suti nyeusi) , akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa Serikali na Chama katika eneo ambalo amepanda mti katika kampeni ya upandaji wa miche ya miti 15,000 katika eneo la Bwawa la Mindu Manispaa ya Morogoro.*



*Vijana wa vikundi vya Boomsate na Twaweza Mindu wakiwa na Pikipiki 37 walizokabidhiwa, zenye thamani ya shilingi milioni 80 zilizotolewa Mikopo ya asilimia 10 ya uwezeshaji wa kiuchumi na Manispaa ya Morogoro katika sherehe za maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani Desemba 01/2020 katika eneo la Stendi mpya ya daladala Mafiga.*



*Wajumbe wa kamati ya Fedha na Uongozi wakiongozwa na Mstahiki Meya Pascal Kihanga(mwenye suti nyeusi) wakikagua ujenzi wa madarasa katika shule ya Sekondari Kihonda.*

# MAGUFULI AWATAKA WAFANYABIASHARA SOKO KUU LA CHIFU KINGALU KUFANYA BIASHARA, WAKATI KERO ZAO ZIKISHUGHULIKIWA.

INATOKA UK... 01

"Niwaombe wafanyabiashara nyinyi ni wazalendo, fanyeni kazi yale mliyoniambia nimewaachia viongozi wangu washughulike nayo, tunataka kuona mkifanya biashara zenu kwa haki bila kunyanyaswa, lakini pia mpendane, suala la mizigo yenu hamtalipa ushuru , mtakacholipa ni bei ya maeneo ambayo mmepangishwa tu, lakini huu ushuru ambao Serikali ilishatoa maelekezo usitishwe haraka, Serikali yangu ipo kwa ajili ya wanyonge , fanyeni kazi msivunje sheria" Ameongeza Magufuli.

Katika hatua nyingine, ameomba Viwanda vilivyokufa viendelee kufufuliwa na vifanye kazi ili vizalishe ajira kwa wananchi na kuiongezea taifa pato katika kufikia uchumi wa Viwanda.

Hata hivyo, amempongeza Mbunge wa Jimbo la Morogoro, Mhe. Abdulaziz Abood kwa uchapakazi wake huku akisema ataendelea kushirikiana vyema na wana Morogoro husuani katika kuboresha huduma ya afya na miundombinu ili kuweza kutumika kujenga uchumi wa Taifa pamoja na Mkoa wa Morogoro ikiwa ni utekelezaji Ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025.

Aidha amewataka wale wote ambao wamekuwa wakishiriki katika tozo kubwa za vizimba na kuwapangishia wengine walipe fedha hizo mara moja kwani Soko hilo limejengwa na fedha za Serikali na sio kwa ajili ya kuwanufaisha watu.



*Mtaalamu Mshauri wa Ujenzi wa Soko kuu la Chifu Kingalu Morogoro Kelvin Chahcha akitoa maelezo yamradi wa soko hilo kwa Mhe. Dkt. Rais John Pombe Magufuli wakati wa uzinduzi wa soko*

Mwisho, amewashukuru wananchi wa Mkoa wa Morogoro kwa kuonesha mapenzi mema ya kumpa kura nyingi za ndio katika uchaguzi mkuu uliopita wa mwaka 2020 na kufanya Morogoro kuongoza kura kwa asilimia 96 katika mikoa yote Tanzania, ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro iliongoza kwa kura kwa asilimia 99.6 kuliko Halmashauri zote nchini .

Waziri wa TAMISEMI, Mhe. Selemani Jaffo, amesema Soko hilo baada ya kukamilika litakuwa na manufaa makubwa ya kuweza kuibadilisha Manispaa ya Morogoro pamoja na ustawi wa maisha yao.

Aidha, amewataka Viongozi wa Morogoro kuhakikisha wanaliendesha Soko hilo vizuri ili wananchi waweze kupata fursa nzuri ya maendeleo.

Kwa upande wa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Loata Sanare, amemshukuru Mhe.Rais kwa kutembelea Mkoa wa Morogoro na kumpongeza kwa ushindi alioupata wa kishindo huku akisema kuwa ushindi wa Mhe. Rais umetokana na kazi alizozifanya katika kipindi cha miaka 5 iliyopita.

Pia amemshukuru Mhe. Rais kwa ujenzi wa miradi mikubwa katika mkoa wa Morogoro ikiwamo mradi wa SGR, Bwawa la Umeme, Stendi ya Msamvu, Stendi ya daladala Mafiga , Soko Kuu la kisasa pamoja na kuboresha huduma za afya,vituo vya afya na miundombinu.

"Mh. Rais umetupa heshima kubwa ya kutupatia miradi mikubwa, tunaamini miradi hii ikikamilika itafanya maendeleo yaende kwa kasi kubwa , tuna miradi mbali mbali ya kimkakati kama Soko hili na mingine, umetupa fedha nyingi za kujenga Hospitali pamoja na vituo vya afya 17 , Ujenzi wa madarasa 257 ambayo yamefikia asilimia 87% , pia tuna changamoto ya ukubwa wa Wilaya zetu ambapo tunaomba uangalie jinsi ya kuzigawa maana ni kubwa sana na kuna muda wananchi wengine wanashindwa kufikiwa, tunajua haya yote umefanya kwa mapenzi yako ya kutaka kuona mkoa wetu unakuwa kiuchumi"Alisema RC Sanare.

Naye Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Mhe. Abdulaziz Abood, amemshukuru Mhe. Rais kwa kuipatia Manispaa ya Morogoro Bilioni 17.6 kwa ajili ya ujenzi wa Soko hilo.

Aidha, amesema licha ya Soko hilo kuwa zuri lakini zipo changamoto nyingi ikiwamo kuzuia Bajaji, bodaboda na daladala kuingia kushusha wateja ndani.

Mbali na hayo, Mhe. Abood amemshukuru Mhe. Rais ,kwa kuipatia Manispaa ya Morogoro fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ikiwamo mradi wa Stendi Mpya ya Daladala mafiga, mradi wa maji wenye thamani ya shilingi Bilioni 185, mradi wa maji Kihonda na Lukobe ambao utagharimu shilingi Bilioni 2.2 ambapo mpaka sasa zimeshatoka shilingi milioni 100 fedha zilizobakia ni Bilioni 2.1 kwa ajili ya kukamilisha mradi huo.



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro Sheilla Lukuba(wa nne kulia) akiwa na watumishi wa Manispaa katika jiwe la msingi mara baada ya uzinguzi wa Soko kuu la Chifu Kingalu*

# WAITARA ARIDHISHWA NA USAFI MANISPAA YA MOROGORO, ATAKA KASI IONGEZWE KATIKA UPATIKANAJI WA DAMPO LA KISASA.

INATOKA UK... 06

kutohudumia dampo hilo ipasavyo kunapelekea uchafuzi wa mazingira, harufu mbaya, na maji yenye sumu kali na kuhatarisha afya ya wakazi wa maeneo jirani viumbe hai na mazingira kwa ujumla.Aidha alisisitiza kuendelea kutoa elimu kwa wananchi jinsi ya kutenganisha taka nyumbani ili waone taka ni dili na sio uchafu mara baada ya kuanzisha kiwanda chenu cha uchakataji wa takataka.

Katika ziara hiyo ameitaka Halmashauri kuwa na mikakati mizuri ya kusimamia usafi ikiwa ni kuwa na mbinu bora za kufanya kila mmoja kuona jukumu la usafi ni lake na kuwa na sheria ambazo zitatekelezwa kwa asilimia mia moja katika usafi ikiwa ni pamoja na tozo za usafi na faini kwa wale waharibifu wa mazingira.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Bakari Msulwa, amesema Wilaya ya Morogoro inakabiliwa na changamoto nyingi za kimazingira lakini wapo tayari sasa kuanza kutekeleza maagizo hivyo watajipanga na timu ya wataalamu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkoa na NEMC ili kuona changamoto hizo zinafanyiwa kazi.



*Naibu waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mwita Waitara akiwa na Watumishi wa Manispaa katika ziara ya kutembelea dampoi Manispaa ya Morogoro*

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, amesema wapo katika hatua za kuhakikisha kwamba Kamati zote za Mazingira zinafanya kazi ipasavyo ili kuondokana na tatizo hilo. Kwa upande wa Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba,amesema Manispaa ya Morogoro imetenga bajeti ya shilingi milioni 300 kwa ajili ya ununuzi wa gari la taka ili kuongeza nguvu katika uondoaji wa taka.

Awali akitoa taarifa ya hali ya mazingira na usimamizi wa taka katika Dampo, hilo, Afisa anayesimamia Dampo, Alex Roman, , amemueleza Mhe. Waitara kuwa, Dampo hilo linakabiliana na changamoto mbali mbali ikiwa ni pamoja dampo kutokuwa la kisasa , idadi ya watu wanaongezeka pamoja na uzalishaji wa taka katika Kiwanda cha Mpunga. Romani, amesema, kwa siku Dampo hilo linapokea tani 180 hadi 200 za taka zinazozalishwa na kuingia katika dampo hilo.

Amesema katika kuhakikisha changamoto hiyo inakwisha, Manispaa ya Morogoro imeandaa eneo Kiegea lenye zaidi ya hekari 1000 ili kujenga Dampo la kisasa.

# HABARI PICHA KUONESHA MATUKIO MBALIMBALI.



*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Bakari Msulwa, (kushoto mwenye suti nyeusi ) , Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa TAMISEMI , Mhandisi Joseph Nyamuhanga (katikati) pamoja na Watumishi ngazi ya Mkoa, Wilaya na Manispaa wakiwa katika picha ya pamoja katika ziara ya Katibu Mkuu wa TAMISEMI alipotembelea Soko Kuu la Chifu Kingalu Manispaa ya Morogoro.*



*Mkuu wa mkoa wa Morogoro Mhe. Loata Sanare( kulia) akizungumza na mfanya-biashara wa nguruka katika Soko kuu la Chifu Kingalu Morogoro katika ziara yake ya ukaguzi wa soko hilo*





*Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood (katikati) akikagua eneo la wafanya-biashara wa mboga na vitoweo Soko Kuu la Kisasa Manispaa ya Morogoro, (kushoto) Mkuru-genzi wa Manispaa ya Morogoro , Sheilla Lukuba.*

# WAZAZI WAASWA KUTOA MALEZI BORA KWA WATOTO ILI KUTIMIZA NDOTO ZAO.

INATOKA UK... 16

wa ikifanya shughuli mbalimbali zikiwemo utoaji wa elimu kwa jamii juu ya ukatili wa kijinsia kupitia Redio ya Dizzim, Redio ya Abood, MVIWATA , utoaji elimu Shuleni pamoja na midahalo mbalimbali ya kujadili juu ya ukatili wa kijinsia kwa wanajamii katika Kata mbalimbali ikiwemo Kata ya Kichangani, K/Ndege, Lukobe na Mwembesongo.

Mwisho amechukua fursa ya kutoa shukrani kwa wazazi , Dawati la Jinsia Polisi, wamiliki wa Makao na Vituo vya watoto wadogo, wananchi na watoto wote waliohudhuria katika kuhitimisha kilele hicho cha Siku 16 za kupinga Ukatili wa Kijinsia.

Kwa upande wa Mtoaji maada kutoka Ustawi wa Jamii Manispaa ya Morogoro, Hamisa Kagambo, amesema wamekuwa wakishuhudia kupokea taarifa juu ya ukatili wa kimwili na kingono kwa watoto wa kike pamoja na Wanawake jambo ambalo amesema ipo haja kubwa ya jamii kupatiwa elimu ili kutokomeza vitendo hivyo.

Amesema , Manispaa ya Morogoro kupitia Kitengo cha Ustawi wa Jamii, imekuwa ikitoa elimu mara kwa mara kwa jamii juu ya ukatili wa Kijinsia.

Kwa upande wa Afisa TAKUKURU Mkoa wa Morogoro, Bigambo Thomas, amesema sababu kubwa inayopelekea ukatili wa kijinsia ni pamoja na mmomonyoko wa maadili , hali ambayo imekuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa kushamiri kwa vitendo vya Ukatili wa Kijinsia katika Jamii.

Bigambo,amesema kuwa katika Ukatili wa kingono waathirika wakubwa wa matukio hayo ni pamoja na wanawake,watoto na wanafunzi , hivyo ametoa rai kwa wazazi kukaa na watoto wao ili kuangalia mienendo yao kwani vipo vitendo wanafanyiwa lakini wamekuwa wasiri sana kuvielezea.

Naye, Mwakilishi wa Dawati la Kijinsia Polisi Kituo Kikubwa Morogoro, Mariam Masalu , amesema watu wanapofanyiwa ukatili wanatakiwa kukimbilia katika Dawati ili hatua ziweze kuchukuliwa kwani bila kufanya hivyo na kujichukulia maamuzi yao wanapoteza ushahidi.

Ikumbukwe kwamba Maadhimisho hayo yameratibiwa na Manispaa ya Morogoro kwa kushirikiana na wadau wa CVM(kirefu chake) ambao wamekuwa wadau wakubwa wa Manispaa ya Morogoro katika kupinga vita ukatili wa Kijinsia pamoja na kutetea haki za Wafanyakazi wa Nyumbani ambao wamekuwa wakiwawezesha katika kufikia ndoto zao.



*Afisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Morogoro, Sidna Mathias, (kushoto) akisalimiana na Mwenyekiti wa Makao ya Watoto ya Multi Dome Relief Centre, Ndg. Fauzi Karama Jumaa( wapili kutoka kulia) mara baada ya kuhitimisha kilele cha Siku 16 za kupinga Vita Ukatili wa Kijinsia.*

# DC MSULWA AHAKIKI WAFANYABIASHARA SOKO KUU KINGALU MANISPAA YA MOROGORO.



*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Bakari Msulwa akizungumza na wafanyabiashara wa Soko kuu la Kingalu katika zoezi la uhakiki wa vizimba na vioski*

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe.Bakari Msulwa, ameongoza zoezi la uhakiki la wafanyabiashara katika Soko Kuu la Kingalu Manispaa Morogoro ambalo limefanyika Februari 13/2021.

Akizungumza na waandishi wa habari, Msulwa, amesema lengo la kuhakiki ni kutaka kutatua changamoto za wafanyabiashara ikiwamo wale waliochukua vizimba zaidi ya kimoja, wapangishaji wa vizimba na baadhi ya watumishi wa Serikali ambao walijihusisha na kuchukua vizimba.

Msulwa, amesema zoezi hilo linafanyika kwa siku 2 ikiwa ni Jumamosi na Jumapili ambapo mara baada ya zoezi hilo taarifa zitawasilishwa kwa Mhe. Rais kufuatia maagizo yake aliyoyatoa wakati wa uzinduzi wa Soko hilo.

Aidha, amewataka watumishi ambao wamechukua wajisalimishe na kurejesha vizimba ndani ya masaa 12 vinginevyo watapoteza ajira zao na kukosa vizimba vyote kwa pamoja.

"Tumelianza zoezi hili leo, mategemeo yangu tutamaliza salama kama wale ambao walienda kinyume na utaratibu watatupa ushirikiano, niwaombe wafanyabiashara tutoe ushirikiano na taarifa ziwe za kweli, tupo hapa kwa ajili ya kutekeleza agizo la Serikali, hatuhitaji mdhaha kama mtu atashindwa ajue tutamfikisha mahakamani ili aongee lugha nyingine zaidi ya hapa, tunachotaka haki itendeke, tunataka kizimba kimoja mtu mmoja, wale watumishi nimetoa masaa 12 umekula pesa zitapike haraka na uturudishie kizimba chetu " Amesema DC Msulwa.

Hata hivyo, amesema kuwa licha ya uhakiki huo lakini ipo kamati iliyoandaliwa kwa ajili ya uchunguzi wa changamoto za soko ikiongozwa na Waziri wa TAMISEMI , Mhe. Suleiman Jafo , Mkuu wa Mkoa, Kamati ya ulinzi na usalama Mkoa, Mkuu wa Wilaya pamoja na Kamati ya ulinzi na usalama Wilaya.

Katika zoezi hilo, pia aliweza kusimamia uchaguzi wa mpito wa viongozi mara baada ya uongozi wa soko kuvunjwa na Mhe. Jafo, ambapo uongozi huo wa mpito utaungana na Kamati kuu ili kushughulikia kero za wafanyabiashara hao.

Mwisho, amepiga marufuku wanaharakati Sokoni huku akisema hao ndio wanaochelewesha maendeleo.

"Sitaki kuona wanaharakati humu ndani, hawa ndio wanatuchelewesha kila kukichwa mabarua wanahangaika na mabarua na kuwashawishi wenzao kuwa na migomo isiyo na tija, ninachotaka ni kuona tunapata uongozi mzuri shirikishi ambao utasimama imara kuhakikisha soko letu linakwenda mbele na malengo ya Serikali yanatimia, Uongozi ni mmoja tu tutakao utaka hawa wanaojiita wanaharakati wakatafute soko lao siwataki humu ndani, nikiwakuta nitawachukulia hatua,tunahitaji kupiga hatua sio kila siku migogoro ambayo wapo watu wachache tu wanao tuharibia"Ameongeza DC Msulwa.

Naye Mstahiki Meya wa Manispaa Morogoro, Mhe.



*Wafanyabiashara wa Soko kuu la Chifu Kingalu wakisikiliza maelekezo toka kwa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Bakari Msulwa wakati wa zoezi la uhakiki wa vizimba na vioski vya Soko hilo*

Pascal Kihanga, amewataka wafanyabiashara kuwa wakweli ili kufanya zoezi hilo kuwa jepesi.

" Niwaombe wafanyabiashara tuwe wakweli na taarifa zetu, hili ni zoezi nyeti sana na ni maagizo ya Serikali ukishindwa kutupa ukweli , ipo sehemu ambapo utaenda kusema ukweli, tunachokitaka sisi kero ziondoke tufanye kazi, Soko hili ni lenu, hatuwezi kufikia malengo kama huku mna minung'uniko , tunataka soko liwe tulivu na malengo ya Serikali yatimie" Amesema Mhe. Kihanga.

Kwa upande wa Mkurugenzi Manispaa Morogoro,Sheilla Lukuba, amempongeza Mkuu wa Wilaya kwa kusimamia zoezi hilo huku akimuahidi kumpa ushirikiano wa kutosha na kupokea maelekezo yatakayotolewa.

Zoezi la uhakiki limehusisha wafanyabiashara ambapo ni waasisi waliopisha ujenzi wa soko jipya wapatao 470,



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro Sheilla Lukuba( kulia) akizungumza jambo na Afisa elimu Sekindari Dkt. Janeth Barongo wakati wa ziara ya ukaguzi wa madarasa mapya*



*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Loata Sanare(kulia) akizungumza na viongozi wa Shule ya Sekondari Sua katika ziara ya kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa.*

# HABARI PICHA KUONESHA MATUKIO MBALIMBALI.



*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Loata Sanare(katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya viongozi wa Mkoa wa Morogoro katika kikao cha kujadili mpango wa usambazaji wa maji vijijini RUWASA*



*Katibu Tawala Wilaya ya Morogoro Ruth John akizungumza wakati wa zoezi la Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Bakari Msulwa Kukabidhi viti na Madawati katika Shule ya Sekondari Kihonda*



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro Sheilla Lukuba(wapili kutoka kulia) akimkabidhi sola mwalimu mkuu wa Shule ya Msingi Ujirani kaya ya Mkundi ili kuwasaidia Walimu kupata huduma ya umeme Shuleni hapo*



**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**
OFISI YA MKURUGENZI
S.L.P 166
**MOROGORO TANZANIA**

(C) 2021